

Mwaka jana nilikuwa wa mwisho darasani.
Wenzangu walinicheka sana,
eti nimeshika mkia.





“Kadogoo, kwa nini
wewe unakuwa wa
mwisho darasani?”
Mwalimu alimuuliza
Kadogoo.



Aliendelea kufikiri
namna ya kubadili
maisha yake.

Aliamua kuchunguza
wenzake darasani.

Aha!

Kumbe wanasoma
vitabu na madaftari.




Alipofika nyumbani,
alimwambia mama
yake angependa
kufanya vizuri
darasani.

Mama alimpa moyo.

Jioni ilipofika alisoma na dada yake.

Dada alimpa maelekezo ya
kusoma na kuandika.





“Soma vitabu vya hadithi, fanya kazi za darasani, uliza walimu na rafiki zako kupata msaada zaidi.” Mama alisisitiza.



Siku zilivyokwenda
mbele. Kadogoo
alijisomea kwa bidii na
pia alishirikiana kwa
ukaribu na rafiki zake
Matata na Jeni.

Wakati mwingine alikwenda
kwa mwalimu kuomba msaada zaidi.

Walimu walimsaidia Kadogoo.






Baada ya muda
walifanya majaribio.

Matokeo yalipotoka,
Kadogoo alikuwa
amefauli vizuri.




Wanafunzi wengine
nao waliongeza bidii
ya kusoma darasani.



Matokeo hayo yalimtia
moyo Kadogoo.

Sasa alijisomea kwa
bidii zaidi na zaidi.



"Wa kwanza alikuwa
Kadogoo!"




Mwisho wa muhula ulipofika,
mwalimu alisoma matokeo ya
mtihani wa mwisho wa muhula.

Wa tatu alikuwa Matata, wa pili
alikuwa Jane na wa kwanza alikuwa
Kadogoo.

Kadogoo aliruka kwa furaha. Rafiki
zake walifurahi pia.

Mwalimu alimpa Kadogoo zawadi
nzuri. Aliwashauri wanafunzi wengine
waige mfano wa Kadogoo.



Nyumbani Kadogoo alipongezwa na dada na mama pia.

“Nitajisomea kwa bidii zaidi.”

Kadogoo alijiwekea ahadi hiyo.

